*Leo ni kwa ajili yetu sote, kwa wale wote watakaotuongoza kuelekea mbele.*

**SURA YA I**
*Vipengele vya Kutafuta*
*—11 —*

**SURA YA II**
*Sauti Zetu*
— 19 —

**SURA YA III**
*Nguzo za Jitihada Zetu*
*—45 —*

I

# VIPENGELE VYA KUTAFUTA



# 1.
# *Kuashiria Njia Mpya*

*"Kila mtu akisaidia kushikilia anga,*
*basi mtu mmoja hatachoka."*
—METHALI YA TSHI

Kama unasoma hii, ni kwa sababu umevutiwa kuhudumia binadamu. Umehamasishwa ufikirie kuhusu mustakabali wa pamoja, uliojengwa na sisi sote kwa ajili yetu sote. Una motisha ushikane mikono na wale walio karibu nawe na wale walio mbali. Uamini. Kuinuka. Utafute njia ya kuendelea mbele.

Kama vile vipengele vyote vinavyoungana kukuza maisha, hivyo ndivyo tunavyopaswa kuleta mitazamo yote pamoja ili kuleta usawazisho na ufanisi katika shirika letu.

# *Lazima tuwe kama maji*

*"Maji hubadilisha dunia. Kadri mawimbi yanavyoinuka, ndivyo maji yanavyozidi kuwa na nguvu, na ndivyo yanavyozidi kuwa na athari kubwa duniani"*

—SAMUEL BIZUMUREMYI

Ni lazima tubadilike ipasavyo ili tuweze kunawiri katika hali zote. Sisi ni chanzo cha nguvu za kudumu na pia furaha na burudani. Nguvu zetu ziko katika upole wetu.

# *Lazima tuwe kama dunia*

*"Dunia inastahimili kila kitu, kila mtu anaweza kufanya chochote humo — na hapo ndipo tunapotaka kufikia sisi kama Alight."*

—ROSINE MPAMYA

Tukiwa tumeweka misingi yetu thabiti, ni lazima tupalilie na tuzidishe kila kitu kinachotokana nasi. Tunasherehekea magugu yanayojitahidi kuibuka kwenye lami, maua yanayochanua wakati wa ukame, kuvu inayopitisha virutubishi katikati ya miti.

# *Lazima tuwe kama hewa*

*"Kimsingi, nafasi hii iliyojaa hoja igeuke kuwa hewa itakayotumika na watu wote watakaoathiriwa na kazi ya Alight."*

—DANNY REARDON

Japo tupo kila mahali, sisi ni nguvu ambayo huchochea maendeleo bila kuonekana. Sisi ni msingi wala si angazio. Tuko wazi katika athari zetu na tunakaribisha kila mtu bila malipo.



# *Lazima tuwe kama moto*

*"Ninaiona Alight kama moto kwa sababu inachoma kwa nguvu na uchu, inaharakisha kutekeleza mipango mipya, lakini inaweza kufifia isipoongezwa makali baada ya muda."*

—MWANDISHI HAJULIKANI

Huku tukiendelea kuwaka kwa uchu wa mawazo mengi makubwa, tunaongezwa makali na kila hoja mpya inayoibuka. Kamwe hatutazuiwa kama taasisi na sheria na misingi ya kufuatwa, lakini tutanawiri kama chanzo cha kudumu na mnara wa taa unaowaka.

# *Lazima tuwe kama anga*

*"Alight itakuwa anga, kwa kueneza imani ya uwezekano katika kila hali kwa ulimwengu wote, na hivyo kujenga nafasi ya ugunduzi na uboreshaji."*

—MARY WANJIRU

Tunakaribisha umati, na upeo wetu hauna kikomo. Ndani yetu, kuna mivutano inayounda mizunguko asilia. Kila mtu ana nafasi ya kutekeleza wajibu wake.



II

# SAUTI ZETU



# 1.
# *Kikumbusho*

*Hadithi imechangiwa na hali walizopitia Teresa Devick, Jacques Prevert Rumanyika na Aphrodice Mutangana*

Kulikuwa na hamu na matarajio makubwa walimu wawili walipoanza kufundisha darasa lao la kwanza. Chumba hicho kilijaa kompyuta, maabara mpya ya teknolojia iliotazamiwa na kutengenezwa na walimu hao hao ambao walisimama mbele ya chumba. Ilikuwa ndani ya kambi ya wakimbizi.

Manusura wa migogoro, vijana hawa walitazamia walimu wao, wakiwa na hamu ya kujaza akili zao kwa mambo mapya, kuongozwa na kuelekezwa kwenye changamoto za mustakabali wenye mafanikio. Kuelekezwa kwa kazi na safari. Walimu hao wawili waliosimama mbele ya darasa, wakiwa manusura pia na wakiwa hawajitimiza umri wa utu uzima, walikuwa wametengeneza maabara hii ili kufundisha darasa la kwanza la usimbaji kwenye jamii hiyo.

Somo lilipoanza na maswali yalipoulizwa kutoka kwa mwalimu hadi kwa mwanafunzi, vijana walijibu kwa mashindano ya kirafiki, kila

mmoja akiongea kabla ya mwenzake kumaliza kwa majibu msisimko ambao haukufikiriwa kwa umakini.

Baada ya darasa hili la kwanza kumalizika, walimu walitazamana na kucheka kwa sherehe na faraja. Darasa lao la kwanza lilikuwa na vurugu, lakini walikuwa wamefaulu. Na angalau wanafunzi walishiriki.

Kisha, kwa majonzi, mmoja akamwambia mwenzake, "Je, umegundua kulikuwa na wanawake wawili tu?"

Mwalimu mwenzake akamjibu, "Ndiyo, na hakuna hata mmoja wao aliyezungumza."

Siku ya darasa lililofuata, walimu wakahakikisha kwamba wamewaita wanawake hao wawili. Na walipoitwa, wote wawili waliwaachia nafasi wanaume waliokuwa wengi. Wanaume waliowanyamazisha bila kusita.

Ilipofika wakati wa darasa lijalo kuanza, walimu waligundua mwanamke mmoja tu ndiye aliyerejea. Kwa hiyo wakatazamana na mwalimu mmoja akawaambia wanafunzi wenye hamu ambao maabara ilitengenezwa kwa ajili yao, "Kama kila mmoja wenu hatakuwa na dada hapa leo, hatutakuwa na darasa."

Na wanaume wote wakaondoka kutafuta akina dada wa kuwaalika.

Darasa lilipoanza tena, lilikuwa na idadi sawa ya wanawake na wanaume.

Na wanawake wakaanza kuzungumza.

Na walisikika.




**TAFAKARI JUU YA HUDUMA YAKO KWA BINADAMU:**

*Kumbuka kilichokuvutia kwenye kazi hii*

*Elekeza mtazamo wako wa kipekee*

*Zingatia mapendeleo yako*





# 2.
# *Nguvu*

*Hadithi imechangiwa na hali aliyopitia Dada Irene O'Neill*

Jioni moja ya mapukutiko, kundi la watawa kutoka maeneo mbalimbali ya eneo hilo waliketi kwenye viti baada ya chakula cha jioni, huku wakinywa chai au bia na wakitazama tukio la michezo kwenye televisheni.

Kina dada hao walifundisha wanafunzi wa shule za upili, na walikuwa wamekusanyika kwa ajili ya warsha ya siku mbili, kujifunza kutoka kwa kila mmoja na wakubwa wao. Ulikuwa usiku wa kawaida, Uliojaa hadithi, michezo ya bodi, na kicheko. Aina ya joto la usingizi lilikuwa limetanda baada ya siku nzima ya kukaa pamoja.

Baadaye kidogo, dada kutoka kwa mkusanyiko wa waliokuwa wamewaalika akaingia chumbani na mwanamke wa umri wa mdogo. Makazi ya wanaonyanyaswa nyumbani yalikuwa yanafungwa. Alikuwa mmoja wa wanawake kadhaa ambao waliishi huko pamoja na watoto wao. Wanawake ambao maisha yao yalikuwa yamesitishwa katika juhudi zao za kurejesha hali ya kujitegemea. Kulinda familia zao. Wote wakiwa na mipango ya kupata nyumba mpya na maisha mapya, lakini bila mahali pengine pa kwenda kwa sasa. Wote wangetupwa nje mwishoni mwa mwezi, zilikuwa zimesalia siku tano

pekee.

Mwanamke huyo alikuwa amekuja kanisani kutafuta joto na kuomba. Hakuwa amefikiria kuomba msaada.

Wale kina dada watawa wakaanza kushughulika.

Akijongea mbele, dada kutoka upande mmoja wa chumba akaanza, "Nadhani najua mahali tunapoweza kukuhamishia. Hebu nipigie simu."

Akaondoka chumbani kisha akarejea. "Nina mahali, lakini tutahitaji vitanda."

"Vingapi?" mwingine akajibu, "Najua mahali tunapoweza kupata vitanda."

"Nitashughulikia chakula."

"Ninaweza kushughulikia jinsi watoto watakavyotunzwa."

Na kwa njia hiyo, muungano huo wa akina dada ukamsaidia kwa urahisi mwanamke huyu ambaye hakutarajia.

Wakati huo huo, bao likafungwa kwenye televisheni. Nadhari ya kila mtu ilirudi kwenye mchezo walipokuwa wakifanyia mzaha na kushabikiatimu yao.

Watawa wawili wakaanza tena hadithi zao. Wakacheka na kushangilia jioni hiyo.

Mwanamke yule wa umri mdogo akaenda nyumbani na chakula, blanketi nzuri na upendo mwingi.

Na siku iliyofuata makazi yakaanza kuhamishiwa mahali papya. Makazi yenye misingi ya uanadada na maelewano.

Makazi ambayo licha ya kuwa mahali pa kulala, yalikuwa pia mahali penye uponyaji.

Mahali ambapo watoto wao walitunzwa salama.

Mahali pa uanadada.




**TAFAKARI KUHUSU USHIRIKIANO WETU:**

*Kumbuka wewe ni mmoja wa watu kwenye timu*

*Kusanya nguvu za aina nyingi ili uunde sehemu kubwa zaidi*

*Gawa uzito ili pasiwe na mtu anayebeba zaidi*





# 3.
# *Moyo*

*Hadithi imechangiwa na hali aliyopitia Ibrahimu Leno*

Baada ya sherehe ya mahafali yake, mwanaume mmoja alimkumbatia ndugu yake kwa muda mrefu. Wawili hao walikuwa wamepitia mengi sana pamoja. Mwongo mmoja uliopita, maisha yao ya utotoni yalikuwa yamevurugwa na vita. Sasa walikuwa wametengana na familia yao na walikuwa wamepoteza nyumba yao, pamoja na usalama na ujasiri usio thabiti aunaotokana na hali ya kuwa na uhakika.

Na sasa, alikuwa katika hali ya kukosa uhakika kwa mara nyingine. Alikuwa amemaliza shule, bila uhakika wa yatakayojiri baada ya hapo.

"Asante kwa kuwa hapa," alisema walipokuwa wakirudi nyuma ili watazamane.

"Ninajivunia sana," kaka yake mkubwa alijibu.

Muda mfupi baadaye, baada ya ukimya wa mawazo, "Nataka kukuonyesha kitu."

Ndugu hao wawili walipanda gari na kuliendesha katika maeneo ya vijijini hadi

walipofikia makazi waliyoyafahamu. Ilikuwa kambi ya wakimbizi, sawa na mahali ambapo kijana aliyehitimu alikuwa amepokea msaada miaka mingi kabla. Ilikuwa kupitia hali hii ya kambi ya wakimbizi ambapo mtu ambaye hakumjua alilipia shule ambayo sasa alikuwa ameikamilisha.

Kaka yake mkubwa alikuwa sasa anafanya kazi katika kambi hii. Mahali hapo paliishi mamia ya maelfu ya watu, ambao walikuwa wamepoteza makao, kama ndugu hao wawili. Sauti zao za furaha zilijaza hewa kama ndege — sauti ya muziki na kicheko kingi na maumivu na ushindi kwa pamoja.

Alipokuwa akiingiai, aliwaona watu aliokua pamoja nao. Papo hapo, akakutana na mchungaji wake wa siku za ujana kabla ya vita, mtu ambaye alikuwa mshauri wake akiwa mvulana. Mchungaji wake akamkaribisha kwa kumkumbatia. "Sote tunajivunia mafanikio yako sana," akamwambia kijana huyo.

Alihisi uhusiano na mahali hapa kama mto ulioelea ndani yake, ukiunganisha maisha yake ya zamani, ya sasa na yajayo. Nyumbani. Alihisi kana kwamba yuko nyumbani. Kama familia.

Akamgeukia nduguye kwa kilio.

"Hapa ndipo ninapostahili kuwa," alisema.

"Tuna haki ya kuwa hapa. Sisi sote tuna haki ya kuwa hapa."

Na huo ulikuwa mwanzo. Jambo zuri, la kushangaza ambalo tumekuja kulifahamu kuwa wito. Na kwa njia hiyo, akapata wito wa kuwatunza watu hawa, mahali hapa. Watu wake, nyumbani kwake. Na sio mahali hapa tu, lakini mahali popote ambapo watu wasio na makao huja pamoja kuanzisha familia zao wenyewe.

Kuonana.

Kusikilizana.

Kuaminiana.

Kuzindua utele kwa upendo.




**TAFAKARI KUHUSU MOYO WA UTAFUTAJI WETU:**

*Kumbuka unawakilisha wale tunaowahudumia*

*Beba sauti za waliopoteza makao akilini mwako*

*Tazama kwenye lenzi ya maisha uliyoyaishi*





# III

# NGUZO ZA JITIHA-DA ZETU

Tukiwa na vipengele hivyo vitano katika akili zetu na sauti za wale tunaowahudumia katika mioyo yetu, sasa tuangazie kazi tunayopaswa kufanya. Ifuatayo ni mitazamo minne ya kiakili ya kuongoza njia yako huku tukiwaalika watu wapya katika familia ya Alight.

**NGUZO ZA KUTAFUTA:**

*Kugundua Mapendeleo Yetu*

*Kutafuta katika Maeneo Yasiyotarajiwa*

*Kuuliza Maswali Bayana*

*Kufuata Maadili Yetu*

# 1. *Kugundua Mapendeleo Yetu*

*“Kila mtu anahitaji kupewa fursa ya kutekeleza uwezo wake.”*
—DOGON SEDIGY NSHIMIYIMANA

Lazima tuelewe kwamba kila mmoja wetu ana mapendeleo yake. Sisi sote. Kwa sababu sisi ni binadamu. Mkusanyiko wa kipekee wa hali tulizopitia, maadili na utambulisho wa kila mmoja hubainisha maoni na mitazamo yetu kuhusu ulimwengu.

Kama timu ni muhimu kuwa na udadisi na kugundua mapendeleo yetu binafsi ili tuwe na uwezo wa kuona mambo kwa mtazamo wetu na pia kuzingatia mitazamo ya watu wengine. Hali hii hutuwezesha kusaidiana — na kuwa na ujasiri kwa njia bora zaidi pamoja.

**MIFANO YA JINSI YA KUTAMBUA MAPENDELEO:**

Jipe muda wa kutathmini mihtasari ya watu watano. Kisha jiulize swali: Ulivutiwa na nini wakati wa kutathmini kila mgombea? Ni picha gani uliyochora kichwani mwako kuhusu vile ambavyo kila mtu alivyo? Anapoishi? Anavyozungumza? Je, dhana hizo ziliathiri vipi muhtasari ulioupendelea?

Katika mchakato wote, fikiria kama mwanasayansi. Tambua maoni mazuri na mabaya ulio nayo kuhusiana na watu. Jichunguze mwenyewe ili uone kama maoni yako yanatokana na majibu yao au mapendeleo uliyo nayo.


**MASWALI YAKO NA YA TIMU YAKO:***

*Fikiria kuhusu wakati ambapo uligundua kwamba una maoni yenye mapendeleo. Ulishughulikia jambo hilo vipi?*

*Fikiria kuhusu wakati ambao kuna uwezekano mkubwa wa kuwa na mapendeleo bila kujua (inaweza kuwa wakati umechoka, una msongo wa mawazo au unafanya kazi nyingi kwa pamoja). Tunaweza kujitahidi vipi kuleta mazingira ambayo yanahakiki dhana tulizopata kabla ya ithibati? Ni tathmini gani ambazo tayari umezifanya?*

*Jadili kuhusu mapendeleo kwa uwazi na wenzako kwenye timu. Mtahimizana vipi katika safari zenu binafsi?*

* Maswali yametayarishwa na Daktari Ramón Pastrano wa ImpactLives™



# 2.
# *Kutafuta katika Maeneo Yasiyotarajiwa*

*"Ikiwa unapata taarifa kutoka sehemu ile ile, ni wazi kwamba haupati watu bora zaidi."*
—BEN AFFLECK

Wakati wa kumwalika mwanachama mpya ajiunge na familia yetu, lazima tuende katika eneo pana. Lazima tuhakikishe kwamba wito wetu unasikika katika kila sehemu ya ulimwengu. Kwamba inasikika masikioni mwa wale wanaotafuta na wale ambao bado hawajazingatia kutafutwa.

Mambo tunayopaswa kuzingatia kabla ya kutoa wito. *Tunawezaje:*

*Kuwafikia viongozi wanaojua moja kwa moja kuhusu hali ya watu kupoteza makao?*

*Kutafuta katika maeneo yasiyotarajiwa?*

*Kutambua uzoefu ambao haujumuishwi kwenye muhtasari wa kutafuta kazi?*

*Kuwahimiza wale ambao wanaweza kujiona kuwa hawana sifa ya kutosha?*

*Kuhamasisha ufafanuzi mpya wa uongozi?*




Mambo tunayopaswa kuzingatia kuhusu jinsi ya kutafuta.

*Tunapaswa kutoa fursa wapi?*

*Tutumie lugha gani kuelezea jukumu?*

*Ni watu binafsi au makundi gani ya watu yanayoweza kuendeleza juhudi zetu?*

*Tutajuaje kwamba tumetafuta umbali wa kutosha?*



# 3.

# *Kuuliza Maswali Bayana*

*"Ni nini tunachotaka* haswa?"
—MARK WHITE

*"Uwezo wa mtu wa kufanya mambo ya ajabu ni muhimu kwake kama ilivyo kuwa na mantiki."*
—PAULO BENNETT

Sisi ni shirika la watafutaji - na tumeletwa pamoja na hamu yetu ya kupata utu katika kila uwanja wa kazi na ulimwengu wetu. Ili kuzindua uwezo mkubwa uliofichwa nyuma ya urasmi wa mahojiano, ni lazima tuulize maswali ambayo yanafika kwenye moyo wa mtu. Maswali ambayo yanatumika kama milango ya uhusiano na uhalisi.

*“Unaweza kuona muhtasari wa kutafuta kazi na unaweza kujifunza mengi kutokana na muhtasari huo. Lakini... lazima ijumuishe uhusiano wa kimoyo.”*
**– DABBS CAVIN**

Hoja za kusaidia kuona njia mpya za kuuliza maswali:

*Angalia maadili na imani zetu kama msingi*

*Fikiria mambo ambayo ungependa kuulizwa katika mahojiano*

*Pata msukumo kutoka kwa hadithi za wale tunaowahudumia*



*“Mawasiliano yanahusu zaidi kusikiliza kuliko kuzungumza.”* **– MARK DAYTON**


Mifano michache ya maswali ya mahojiano:

*Mara ya kwanza ulipogundua kwamba sauti yako ni muhimu ilikuwa lini?*

*Tuambie kuhusu wakati uliona kitu fulani kizuri kwa mtu fulani na ukasaidia kukinawirisha.*

*Tuambie kuhusu wakati ulipata mwangaza gizani.*

*Fafanua ulimwengu ambao ni tele.*



# 4.
# *Kufuata Maadili Yetu*

*"Tunashughulikia mambo tunapoamini kikamilifu.*
*Na Alight inakusudiwa kuwa chombo hicho cha imani."*
*—ANGELA EIFERT*

Tunapotazama nje kwa mustakabali mpya wa ujasiri wa shirika letu, ni muhimu pia kuangalia ndani. Kuweka msingi wetu katika maadili, imani na lengo la kiini chetu — na kuruhusu mambo hayo yawe nguvu zinazounganisha jumuiya yetu ya ulimwengu mzima.

*Shirika letu limejaa watu wengi wa ajabu.*

*Utofauti huu ni mojawapo ya nguvu zetu kuu.*

*Na mojawapo ya mambo makuu tunayojivunia.*

Na wakati sisi ni nelibini ya vipawa, nguvu na mambo ya kipekee tuliyoyapitia, kuna seti ya maadili yanayotuunganisha sote. Inaendesha jinsi tunavyofanya kazi yetu, jinsi tunavyoingiliana na watu tunaowahudumia (na wenzetu), na inatusaidia kufanya maamuzi. Ni matarajio yetu ya kila mmoja na pengine hata kile ambacho tunaweza kuwajibisha kila mmoja wetu nacho. Labda.

**MAADILI YETU**

## Kuongozwa na Utu

## Kuwa Mtu Bora kwa Ujasiri

## Chochea Furaha

## Chagua Matumaini

## Anza kwa Kutoa

## Tafuta Wengine

## Fanya Yanayowezekana

*Kila kitu tunachofanya kinaegemea imani tatu za msingi ambazo tunashikilia sana. Imani hizi zinaunga mkono maadili yetu, lengo letu, kila hatua tunayochukua na kila maamuzi tunayoyafanya.*



Tunaamini kwamba kuna haki rahisi ya binadamu katika nafasi ya kujenga maisha.

Tunaamini katika ulimwengu wenye utele wa watu wa ajabu ambao wako tayari kusaidia.

Tunaamini katika kufanya jambo bora zaidi.


WRD 5K
495
WRD 17

# *Kuendelea mbele*

*"Alfajiri mpya hunawiri tunapoiweka huru.*
*Kwani daima kuna mwanga,*
*ikiwa tu tuna ujasiri wa kutosha kuuona.*
*Ikiwa tu tuna ujasiri wa kutosha kuwa mwanga huo."*
*——AMANDA GORMAN*

Tunawashukuru kwa kuwa njia ya ujasiri inayoongoza safari ya mustakabali wetu. Kwa kupanua familia yetu. Na kwa kutuongoza daima, pamoja, kwenye nuru.